



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MJI MASASI



Unapojibu tafadhali taja:

KUMB. NA. L.10/I/VOL.IV/76

Tarehe: **01/04/2022**

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Halmashauri ya Mji Masasi kwa kushirikiana na jimbo la ENZIKREIS la nchini Ujerumani inapenda kuwatangazia wananchi wote Raia wa Tanzania kuomba nafasi za kazi kwa mkataba wa miaka miwili kwa nafasi ya;

AFISA MAZINGIRA (NAFASI MOJA).

A. SIFA ZA MUOMBAJI

- i. Awe raia wa Tanzania mwenye umri kati ya miaka 18 – 45
- ii. Awe na shahada ya Mazingira Kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali.
- iii. Awe na shahada ya Usimamizi wa Mazingira Kutoka vyuo vinavyotambulika na Serikali.

B. KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kusimamia wanachi juu ya kudumisha usafi katika maeneo yao ya makazi na biashara.
- ii. Kukusanya takwimu na taarifa mbalimbali zinazohusu usimamizi na hifadhi ya mazingira.
- iii. Kutoa (disseminate) Elimu ya hifadhi ya Mazingira kwa wadau mbalimbali.
- iv. Kufuatilia na kuainisha maeneo yanayopaswa kuhifadhiwa.
- v. Kupitia na kushauri kuhusu utekelezaji wa sera, Sheria ya Mazingira na Miongozo na Mikakati mbalimbali kuhusu Usimamizi na Hifadhi ya Mazingira.
- vi. Kuandaa taarifa ya hali ya Maingira nchini (State of the Environment Report)
- vii. Kupitia na kushauri kuhusu taarifa za tathimini ya athari kwa Mazingira (Environmental Impact Assessment) na Mpango mkakati wa tathimini ya mazingira (Strategic environmental Assessment).
- viii. Kuandaa na kuratibu utekelezaji wa mikakati ya matumizi salama ya tekinolojia ya kisasa (biosafety).
- ix. Kupendekeza miradi ya hifadhi ya mazingira.
- x. Kubainisha na kupendekeza masuala ya mazingira ambayo yanapaswa kuhuishwa katika mipango ya kissekta.
- xi. Kutoa mapendekezo kuhusu utekelezaji wa Sera na Sheria nyingine zinazohusiana na usimamizi wa mazingira.
- xii. Kutoa ushauri kuhusu maeneo yaliyoathirika kutokana na shughli za uchumi zisizo endelevu (kama uchimbaji madini, kilimo, Ujenzi, ufugaji, n.k).

Kiwango cha mshahara kitakuwa TGS D.

FUNDI SANIFU UMEME NA SOLAR (NAFASI MOJA (1))

A. SIFA ZA MUOMBAJI

- i. Awe Raia wa Tanzania mwenye Umri kati ya Miaka 18 – 45
- ii. Muhitimu wa kidato cha Nne (iv) katika masomo ya Sayansi na kufuzu mafunzo ya Mwaka Mmoja katika moja ya fani za Ufundi wa umeme kutoka chuo kinachotambuliwa na serikali au.
- iii. Muhitimu wa kidato cha IV mwenye cheti cha majaribio ya ufundi hatua ya II kutoka chuo cha ufundi katika moja wapo ya fani ya ufundi

B. KAZI NA MAJUKUMU

- i. Kufundisha na kufanya kazi za marekebisho ya Mifumo ya Umeme na Solar.
- ii. Kufundisha wananchi Technologia na Ufundi
- iii. Kusimamia utekelezaji wa sheria kanuni za nishati
- iv Kuandaa ripoti za utekelezaji wa miradi.

Kiwango cha mshahara kitakuwa TGS B.

MASHARTI YA JUMLA

- i. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania
- ii. Waombaji wote waambatanishe vyeti vya shule na taaluma na cheti cha kuzaliwa (certified copy)
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayo jitosheleza yenye namba za simu za wazamini
- iv. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya kiswahili au Kingereza
- v. Uwasilishaji wa taarifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- v Waombaji wawasilishe picha mbili (passport size)
- vi Watumishi waliosimamishwa kazi kwa mashauri ya kinidhamu au waliofukuzwa kazi hawaruhusiwi kuomba.

NB: Waombaji wote mnatahadharishwa kujiepusha na matapeli wanaojitambulisha kuwa wao ndio waajiri na kukutaka utoe rushwa

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **08/04/2022 Saa 9:30 Alasiri**

Maombi yote yatumwe kwa Anwani ya: -

MKURUGENZI WA MJI,
HALMASHAURI YA MJI MASASI,
S.L.P 447,
MASASI


Elias R. Ntiruhungwa
MKURUGENZI WA MJI

MASASI